

REPUBLIC OF KENYA
COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THE HANSARD

Monday, 20th June, 2016

The House met at the County Assembly Chambers, Malindi Town, at 2.30 p.m.

[The Speaker (Hon. Kahindi) in the Chair]

PRAYERS

COMMUNICATIONS FROM THE CHAIR

REMOVAL OF HON. CHRISTINE FONDO FROM ALL PARTY POSITIONS AND HOUSE COMMITTEES

The Speaker (Hon. Kahindi):Hon. Members, I have some communications to make. The Office of the Speaker of County Assembly of Kilifi has received a letter from Kenya Africa Democratic Union (KADU) ASILI. The same has been directed to hon. (Ms.) Christine Gona Fondo who is a nominated Member of KADU ASILI in the Kilifi County Assembly. I will read the letter as follows that:

“Dear Madam, removal from all party positions and House Committees of the County Assembly. The National and Kilifi County officials are still very disappointed because you are still going to other parties meetings despite our warning letter on the issue of your advocacy and association for and with other party and neglecting the issues of KADU ASILI.

Remember, it was already pointed out to you that your conduct of late has not been in the best interest of the party on whose ticket you were nominated. You are still advocating for other parties despite two warnings that you have received.

Your actions are tantamount to insubordination and contempt of the KADU ASILI authority vested in the National Executive Committee (NEC). This behavior has been pointed out to you in our earlier letters both constitute an offence under the Political Parties Act, 2011 part 2 section 14 subsection 5 (e) and (f) as well as under the party Constitution on the Article relating to rights and duties of members.

You were summoned to the disciplinary committee so that a decision could be made on your de-gazettement as a nominated Member of the County Assembly and replace you with someone who has respect for the party and its officials. In the said meeting, you never satisfied the Committee on the reasons which made you support another party. Let it be known to you that this behavior you are exhibiting is bringing disrepute and embarrassment to the party. The NEC has therefore decided to adopt the recommendations of the disciplinary committee and with immediate effect, stripped you of the positions you hold in the party, both at the national and branch offices including, but not limited to the position of the National treasurer.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

By copy of this letter, we are instructing the County Assembly Clerk and Speaker to note and remove you from membership of all committees of the Assembly forthwith.

Note that, should it come to the notice of the party that you are still embarrassing the party by supporting other course of other party or commit an offence bordering on ridiculing the party, the NEC will not hesitate to expel you from the party membership altogether. Yours faithfully, Dr. Abeid .J. Kombo, Deputy Secretary General KADU ASILI”

Hon. Members, having received that letter, I am supposed to direct the Office of the Clerk that the said Member be removed as demanded by the political party and not by the Speaker or office of the Clerk, and the same should be communicated to the finance office, because by virtue of reading this letter before this County Assembly, automatically she is not able to attend any Committee meetings and any privilege that would have otherwise been obtained as a Member of that political party has since forthwith seized.

DEMISE OF NOMINATED MEMBER OF COUNTY ASSEMBLY, HON. (MS.) GRACE CHIHANGA

Hon. Members. today is a sad afternoon because I stand before you to state that the County Assembly of Kilifi last week lost one of its Members; that is hon. (Ms.) Grace Chihanga. She passed on while undergoing medication at Pandya Hospital.

The County Assembly of Kilifi is working together with her family to ensure that the hon. Member gets a dignified send-off. The burial arrangements are so far in progress and a special committee has been constituted today that consists of the family Members, staff of the County Assembly, Members of the County Assembly and representatives from the Office of the Governor. Further details will be relayed to you by the Committee.

On this note, I therefore want to call upon all the Members of the County Assembly to rise up and observe a minute of silence in honour of our fellow hon. Member.

(Hon. Members stood up in their places and observed a minute of silence)

Thank you. I will also give 20 minutes after my communication before any other Business for hon. Members of the County Assembly to eulogize hon. (Ms.) Grace Chihanga. I remember the last time she came to my office, among the very many words we talked about was the opening of the new Chamber. It is really unfortunate that... though we loved her but I think God loved her most. She was one of those persons to sit in this new Chamber but I think that is something which is beyond your control. So after my communication, I will dedicate 20 minutes for any Member who wishes to say something about hon. (Ms.) Grace Chihanga and we all pray that she rests in eternal peace.

VISITING MOMBASA COUNTY ASSEMBLY MEMBERS OF THE COMMITTEE ON ENERGY, TRADE & INDUSTRIALIZATION

Next is that hon. Members, today we are privileged to have special guests who are currently sitting at the Speaker’s Gallery and these are none other than Members of the County Assembly of Mombasa from the Committee of Energy, Trade and Industrialization. As a practice here in Kilifi County Assembly, I will take this opportunity to honour their presence and I will

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

require that if I mention your name hon. Members, you rise up for the Members of the County Assembly to acknowledge you. We have:

1. Hon. Ibrahim A. Kondo
2. Hon. Kibwana S. Baya
3. Hon. Abubakar R. Kibwana

The Members are accompanied by:

1. Juma Baya
2. Mohamed Juma
3. Jamal Omar Awadh
4. Roselyn Randi
5. Rashid Kaka
6. Emily Sialo
7. Leah Simon

Thank you very much hon. Members for paying us a visit and I am hoping that you will have a good time as you sit at the Speaker's Gallery. I will also give an opportunity for hon. Members to acknowledge and welcome our colleagues from Mombasa.

VISITING STUDENTS FROM MAJAONI SECONDARY SCHOOL IN KILIFI

Other than hon. Members from Mombasa, hon. Members of the County Assembly, we are delighted to have students who are visiting from Majaoni Secondary School. Equally, I will mention their names and when you hear your name as tradition here you just stand up so that the Members of the County Assembly acknowledge your presence and then we proceed. We have;

1. Faith Mwarabu
2. Dama Wanje
3. Jimmy Ponda
4. Evaline Gambo
5. Salama Mshele
6. Kazungu M. Mackson
7. Kalango Eunice
8. Saidi N. Kahindi
9. Jackson R. Ziro
10. Emmanuel Amani
11. James Walter
12. Moses Chulah
13. Evans Safari
14. Michael Sifa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

15. Khamis Ryan
16. Deche Nicholas
17. Moses Mvera
18. Thomas Ngonyo
19. Isaac Mjimba Kahindi
20. Ngowa George Nyale
21. Masha Charo
22. Salim Vidzo
23. Erick Kahindi
24. Kazungu Amos
25. Hamis Sulubu
26. Anderson Fikiri
27. Halima Kazungu
28. Sylvia Kafadzi
29. Joyce Kazungu
30. Jacob Mwambire
31. Jerald Mbaruk
32. Geoffrey Katana
33. Zablon Mwamunda
34. Nawaz Ramadhan
35. Erick Mjomba
36. Makanjira Yohana
37. Kwicha Harrison
38. Malcas Khonde
39. George Baya
40. Onyango Fredrick
41. Danson Kiyeye
42. Erick Suileman
43. Tsofwa Alex
44. Chenda Charo
45. Amina Ndoro
46. Evelyn Sada
47. Humphrey Charo
48. Grace Charo
49. Gift Kahindi
50. Gideon Mwamure
51. Erick Kahindi

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Students are accompanied by;

1. Mr. Maina M. Charles - History teacher
2. Madam Halima Aziz - Head teacher

Again, I take this opportunity to welcome you to the newly refurbished Chamber of the County Assembly of Kilifi. I know students you will have a lot to learn in this new era of devolution.

Hon. Members as I take a seat, I would want to first give the opportunity for the Members to welcome the Members of the County Assembly (MCAs) of Mombasa then I will give another opportunity for Members to welcome the students, then we will have 20 minutes to eulogize our departed Member and then we will resume to normal Business of the House. Thank you very much.

Hon. Kaunda: Asante mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuleta makaribisho. Nataka kusema kwamba mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kawi tumetembelewa na Kamati ya Kawi pamoja na Biashara na Viwanda kutoka Mombasa. Kusema kweli, tumekuwa na kipindi kizuri wakati walipokuwa wameingia kumbuka umewakaribisha vyema tulipokuja katika ofisi yako pamoja na ile ya katibu.

Yale ambayo tumezungumza katika kikao kile tangulizi tumeona kwamba ni muhimu kuwa na vikao kama hivi vya Kamati za Bunge za kaunti, kuweza kutembeleana ili kwamba tuweze kuhamasishana na kuweza kujua maendeleo yale yaliyopo. Na pia, tuweze kubadilishana mawazo ili kaunti hizi ambazo katika mfumo huu wa ugatuzi ziweze kufaidi upande wowote ule.

Kwa hivyo mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba katika Kamati hii ya Viwanda pamoja na Kawi na Biashara ikiongozwa na mheshimiwa Ibrahim. Mimi nawakilisha kamati ya Kawi lakini yuko mheshimiwa daktari Mzungu Chitibwi ambaye anawakilisha mambo ya Biashara na mipangilio ya kiuchumi ili naye aweze kupata nafasi na kuweze kuongea. Tunawakaribisha sana wenzetu kutoka Mombasa Kaunti na msikomee hapo. Mzidi kuja ili tuweze kubadilishana mawazo na sisi pia tukipata nafasi tuweze kuja na kuweza kubadilishana mawazo. Karibuni sana. Asante mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes, hon. (Dr) Chitibwi.

Hon. (Dr.) Chitibwi: Thank you very much hon. Speaker. I stand to welcome our guests, hon. Members from Mombasa County to Kilifi County. Welcome to the Assembly. As Kilifi County, we have always been looking at Mombasa as our bigger brother and we thank them for having made us ... in the economy of the Coast counties.

There are very many things which we depend on Mombasa and I would like to say you have not let us down so far. Now as counties, we are endeavoring to come together as an economic block and as a big brother or sister to take your lead; take your part.

It is also good we have students visiting at the same time they are now seeing what we intend to do as counties. Coming together using the economies of scale we can do a lot; it is just the beginning and I believe there are very many projects and endeavors that we can come together towards the people of Coast. Thank you very much that you are here today. I will also come to learn from you. Thank you.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you.

Hon. Mwambire: Thank you very much. Mr. Speaker, as I take this opportunity to welcome our brothers and sisters from Mombasa. Though my elder brother hon. (Dr.) Mzungu has shared that Mombasa is a big brother, I consider them as the same; we are just the same. Mr. **Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Speaker, we are sharing almost everything in Mombasa because they have Nyali Bridge, we have Kilifi Bridge; if they celebrate the Makupa Causeway we have our Sabaki Bridge and we share Mtwapa Bridge. So I do not think we have so many things that we do not share.

What is important is looking at the co-existence between these two counties. Mombasa, despite the fact that they have KPA (Kenya Ports Authority) most of the things we share together. Most of our staff in Kilifi live in Mombasa and most of the staff in Mombasa live in Kilifi particularly Mtwapa. Most of the things we do share together and I believe even through their visit in this county, they will be learning a lot including this Chamber because if we visit theirs it will not resemble ours.

Now that we have shown them the way, I believe they will be planning and they will be visiting us as an equal brother and get more facts on how best they can come up with an either equal or a more comprehensive Chamber than this one.

Mr. Speaker, I salute them for hosting the Headquarters when we had the Provincial Administration and they have a lot of investments in their county but I believe most of the things that they are doing we should also buy from them especially the way they are conducting their traffic among other issues of enforcement. I believe there are some things that we need to learn from Mombasa so that we can also adopt as we streamline our affairs. So do not feel that we are boasting because of having this state-of-the-art Chamber but we are also buying a lot of your ideas. I believe from this time, even other Committees will visit Mombasa so that we can share how best we can take the Coast region forward. Thank you very much Mr. Speaker. I welcome our brothers and sisters and urge that we keep on working together.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Foleni. You can now welcome the students as well.

Hon. Foleni: Hon. Speaker, I want to take this opportunity to welcome my beloved students from Majaoni secondary school. Hon Speaker, Majaoni secondary school is within my Ward and I would like to report to this House that it is the most disciplined and most hardworking school in Kilifi North. So, I have no reservation but to say welcome and may you please take whatever you are going to learn from this institution to your respective areas.

Hon. Speaker, the late Nelson Madiba Mandela once said education is the most powerful tool that is able to change the world. I want to extend this to our beloved students that they should take that quote with a lot of vigour so that one day, one time, they can also be in a position to compose their own quotes because I believe they have the brains to do so. Hon. Speaker, as I conclude in welcoming Majaoni secondary school students, I want to leave them with a verse so that when they leave here, they can be able to memorize this Holy verse in the Bible and in so doing, the same verse will equip them with the relevant knowledge. I want to say that after here, students go and read Proverbs 4:13. Once again, welcome. Thank you.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Foleni, you know you should have proceeded to say what that verse says...

(Laughter)

No you do not have to... on a light note ...it's okay.

Hon. (Ms.) Chiku: Thank you Mr. Speaker, Sir. I rise to welcome the Members of Mombasa County Assembly, please feel free and we thank you for coming to benchmark in our County. Mombasa County is our neighbour bordering Kilifi and Mombasa at Mtwapa. I am truly

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

delighted Mr. Speaker, Sir, for their trip here. Being a Member of the Planning Committee, I do not have to say much but thank you very much indeed.

Mr. Speaker, allow me also to acknowledge Majaoni secondary school. I come from Majaoni and I am a neighbour to that school. It is very good for the young children to be enthusiastic to come to such an institution and see what their leaders are doing. I am sure this Chamber is the envy of the entire 47 counties Mr. Speaker. Thank you very much Majaoni secondary for visiting this place and I hope one day one of you will be sitting in this Chamber. Thank you.

(Applause)

Hon. Hassan: Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii muhimu. Kwanza, nataka kuchukua nafasi hii kukaribisha ndugu zetu, waheshimiwa kutoka Kaunti ya Mombasa ambao ni majirani na kuna sawazisho tu moja ambalo naona kama tumesahau; kwamba, sisi ndio wenye ziwa wao wanalokunywa maji. Naongea kama mwenyekiti wa maji. Kwa hivyo, si kwamba ati ni wakubwa zetu ama ni kiasi chetu. Mimi kwa upande wangu nasema ni wadogo zetu kwa sababu mwenye lile ziwa ni kama vile mfano wa mama, si ndiye ananyonyesha mtoto? Kwa hivyo, karibuni sana ndugu zangu kutoka Mombasa tutashirikiana sana kwa mambo mengi. Vile vile, nataka kuchukua fursa hii kuwakaribisha vijana kutoka Majaoni ambao ni jirani zangu kutoka Wadi ya Tezo. Kwa hivyo jisikieni mko huru. Karibuni sana.

Hon. (Ms.) Mbeyu: Thank you Mr. Speaker, Sir. I rise to give support and welcome the Mombasa County Members to this Chamber. Let them feel at home although Mombasa does not have such a chamber but you can copy us and take this information back home.

Mr. Speaker, I want to take this opportunity to thank the delegation and pass our regards to Mombasa and more so Governor 001 for the support he brought to us during our by- elections in Malindi Sub-County. Thank you so much.

May I take this opportunity to welcome Majaoni secondary students. Mr. Speaker, Majaoni is a neighbour to Kibarani and most students from my Ward learn in this institution. Congratulations and welcome to the Chamber. Thank you.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you. Hon. Members, now we have our 20 minutes to eulogize hon. (Ms.) Grace Chihanga.

Hon. Mwathethe: Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity to eulogize hon. Chihanga. Mr. Speaker, you will have noted that I was going on and off because I was struggling at least to be the first in giving the eulogy. Mr. Speaker, it is with a lot of sorrow and disbelief that I received the news of “home- going” of our beloved sister hon. (Ms.) Chihanga. I remember the day I was in hospital when she was in a comma and I was not able to see or even talk to her. I spent about six hours in vein. The following day, I received the news that she had passed on. It is very sad and painful; it could have been the second person to have left us.

I remember the time when I was also shot twice on the head Mr. Speaker. I only survived death by a whisker and I would also have gone myself. It is only through the mercy of God that I am still standing here. Now, to remember that I survived and another person did not make it really pains me so much but what can we do? When the time has come, we have no choice but to follow the norm that we are here and we are only a passing cloud once the time comes, we shall have to leave.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mr. Speaker, however I know I may be out of order but there is unconfirmed information that hon. (Ms.) Chihanga used to have family troubles that maybe included wife beating which might have contributed to her death. I would ask if this Assembly and the leadership of the Assembly can do something to get the hospital report so that we can come to know exactly what caused her death. We understand that she went through an operation that may have been successful or maybe not because thereafter she changed hospitals and was in a comma until the time she died. It could be that the beating led to the operation which led to her death. I would humbly seek that the hospital report is availed to us to quash the fears and rumours that are coming out. In this regard, I stand to salute and pray that God rest her soul in eternal peace. Thank you.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you hon. Mwathethe.

Hon. Sadi: Nashukuru mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii nami kumkumbuka marehemu Grace Chihanga. Nimemjua marehemu nikijiunga na Bunge hili na siku nilizowahi kujuana naye katika Bunge hili, sikumuona marehemu akiteta na mtu wala akizungumza na mtu kwa ubaya, ama akiwa katika hali yoyote mbaya na mtu. Hii ni kuonyesha marehemu aliishi na watu kwa njia nzuri na kwa upendo. Sisi binadamu sote tuko katika safari na Mwenyezi Mungu amejalia mwenzetu ametutangulia katika safari. Hivyo ni kumaanisha kwamba sisi sote nasi itakapofika wakati wetu tutakwenda aliko.

La msingi ni kwamba binadamu anapoishi na wenzake aishi mfano alivyoishi marehemu Grace Chihanga; tuishi na mwenzake kwa uzuri na kwa upendo ili tunapokwenda mbele ya Mwenyezi Mungu akatuhesabu kama watu wema katika dunia hii. Kwa hayo macheche nasema asante na Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema palipo na watu wema.

Hon. Kombo: Thank you for giving me this opportunity to pay my last respect to our late hon. (Ms.) Grace Chihanga on the Floor of this House. I met the late here though she was married a few kilometers from my homestead. I knew her as a jovial Member of this County Assembly. We ate, played, shared views and made contributions together in this House. We will all agree that the late Chihanga had striking beauty. She was attractive both physically and from her heart. She was sociable and mixed with people easily and for that reason I stand here to pay my last respect in this House and pray that God He rests her soul in eternal peace.

Hon. (Ms.) Christine: Asante kwa kunipa nafasi hii nami kumkumbuka mheshimiwa Chihanga. Nilimjua Chihanga kabla ya kuingia Bunge hili. Tulijuana Nairobi wakati alikuwa na mambo yake na chama chake. Tulipoingia Bunge, alikuwa rafiki wa karibu na alikuwa mcheshi na hakuwa mtu wa hasira kama vile wenzangu walivyosema. Ungemwambia chochote na hatachukua na hasira yoyote. Vile vile, alikuwa mwanakamati wa kamati ya Afya na wakati huo nikiwa mwenyekiti mdogo mara nyingi nilikuwa nikimtafuta wakati hakuna idadi inayohitajika. Kwa hili tutamkosa sana Kamati ya Afya kwa wale waliobaki katika hiyo Kamati. Na pia ni mtu embaye... Siwezi endelea zaidi ya hapo isipokwa ni Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Hon. (Ms.) Zawadi: Asante sana. Nami nasimama kutoa risala za rambirambi kwa mheshimiwa Grace Chihanga. Nilimjua Chihanga wakati majina yetu yalipotoka kwa uteuzi nikawa namtafuta kwa sababu majina yake yamefanana na Grace Mbodza kutoka Kilifi. Wakati tulipokuwa tukiwasiliana ilifikia wakati nikaingia kwa ofisi ya wanachini wa Gavana kuulizia msichana wa Kaloleni na nikaambiwa ni Grace yule pale ndio tuliwasiliana kwa mara ya kwanza. Juzi tulipopokea habari za kifo hiki siku ya Alhamisi, tulikuwa kwa Kamati ya PIC/PAC. Yeye akiwa mwanachama tulishindwa kukaa katika kikao kile kwa sababu ni kiongozi

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ambaye ni mcheshi kwa kila mmoja na tunaona kwamba tutamkosa kwa mambo mengi kwa sababu yeye pia ni kiongozi wetu wa michezo. Michezo yote inayokuja hapa Bungeni yeye hujitolea na yeye sio mvivu. Kwa hakika tukiwa na huzuni kwa sasa katika Bunge letu la Kilifi tunaombea roho ya marehemu Grace Chihanga mwenyezi Mungu ailaze mahali pema alipojichagulia yeye mwenyewe.

The Leader of Majority (Hon. Mwingo): Mr. Speaker may the Lord rest the soul of hon. (Ms.) Chihanga in eternal peace. On behalf of people from my Ward, that is Mtepeni Ward and Kilifi South Constituency as a whole, may I take this opportunity to give my condolences to the family of the late hon. (Ms.) Chihanga. I came to know her in this County Assembly after she had been nominated. For the time we have been together in this Assembly, she has really been proved to be social to everybody. She has been active in the Orange Democratic Movement (ODM) party.

We recently had a by-election in Malindi and I understand she played a big role towards the success of the current MP. Hon. (Ms.) Chihanga will be remembered by many. As far as I am concerned, we used to joke. Before her death, she had started teaching me how to hug somebody. Hugging was not my hobby but through her, I was almost developing interest on how to hug fellow hon. Members. I take this opportunity to say we have lost someone who had passion with almost everybody. It is very sad for this House to lose such an important hon. Member.

Hon. Mwambire: Mr. Speaker, it is very sad that I have risen to give my condolences especially on behalf of the ODM party. I knew Grace before coming to this Assembly especially when we were campaigning during the 2013 elections. Grace was an outgoing person. It was very hard for one to pick a quarrel with Grace who was easy to forgive. She was someone who could make friends any time. I remember when I led a delegation to India for a study tour where Grace was the one who brought the colleagues from Nyamira and made us to be close friends and we have been consulting widely with Nyamira County Assembly simply because of hon. (Ms.) Grace's interactions.

Mr. Speaker, I remember on 13th August last year when the Governor called me. He wanted to be represented at the Mekatili wa Menza festival in Magarini. It was a very short notice but when I gave her a call, she accepted to accompany me alongside the chairperson hon. (Ms.) Elina Steven Mbaru and hon. Gibson Matano and we spent the whole day in Magarini as one of the Governor's representatives.

Mr. Speaker, I remember on the first day I had a very difficult morning because I received a call very early in the morning from my colleague hon. Mwayaa telling me that Grace was no more but he restrained me from revealing that information because the hospital had some guidelines to follow before releasing that information. Even at some point, I was compelled to reveal that information to the Clerk but later on I had to call him to restrain him from informing other Members because the hospital wanted to clarify that it was true that she had gone.

Mr. Speaker, there is nobody who can say that somebody is no more and all of a sudden he/she is alive and that is why at the end I had to release that information. I know it is very difficult for me to proceed with eulogizing my sister but God has had a purpose to restrain our beloved Member from joining this Chamber. With those few remarks, I pray to God to place the soul of our beloved sister in internal peace. Amen.

Hon. Mwayaa: Asante sana Mheshimiwa Spika. Nami nimesimama kutoa rambirambi zangu kwa familia ya marehemu dada yetu Grace Chihanga. Kusema kweli, Chihanga anatoka kwa Wadi yangu alikuwa ameolewa kule na nilivyomjua marehemu Grace Chihanga ni wakati

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

nilivyokuwa mwenyekiti wa Baraza la mji wa Mariakani yeye alikuwa akifanya kama CHW katika hospitali ya Mariakani yaani *Community Health Work*. Kabla aje Bunge letu la Kilifi, nilimjua kwa huo mda na tuliona jina lake kuwa ameteuliwa miongoni mwa wale waliotakiwa kuja kufanya kazi huku na mimi nikawa nimebahatika kuchaguliwa na watu wangu wa kule Kayafungo.

Tulikuja tena tukaonana huku na tumefanya kazi ikiwa mimi nimefanya kazi na yeye katika kamati mbili; Kamati ya Uwekezaji na ile ya Afya. Juzi nilivyosikia ni mgonjwa zaidi, nikachukua hatua nikaondoka hapa saa kumi na nusu kuelekea kule sehemu za Pandya na tukangoja maana tulifungiwa nje ili kwamba daktari aje. Alivyofika daktari kutoka hospitali ya Mombasa akasema, *'The lady is very sick'* hilo ndilo neno alilotumia lakini mimi sikutaka kujizuia pale nje nikaingia mpaka ndani nikamuuliza ni mgonjwa kiwango gani. Maana vile nilikuwa nimemuona pale kupumua kwake kulikuwa ni kung'ang'ana nikajua labda ni mashine ile ya ICU. Nikauliza maswali mengi lakini mwisho, yule daktari wa hospitali ya Mombasa akasema kwamba hawezi kutamka maana Pandya kuna mwenyewe labda yeye ndiye atatamka lakini ametuacha. Ndio maana nikachukua hatua hiyo nikamjulisha Naibu Spika wetu, na hata wewe nilijaribu kukufikia kwa simu lakini sikuweza.

Nilikuwa na watu wa jamii yake maanake ni watu wangu kule ambako aliolewa tukazungumza mengi na baadaye tukaweza kupeleka ule mwili wa mwendazake mheshimiwa pale kwenye chumba cha kuhifadhia maiti. Tutamkumbuka maana kamati zangu mbili zimepata pigo na pia nimemjua kwa mda huo wote tangu akiwa CHW kule Mariakani na hata zile zawadi nyingi tumezipata kama wenzangu walivyosema, wakati tukiwa Eldoret, yeye alichangia pakubwa maana alikuwa anacheza *netball* na pia michezo mingine. Mimi kufikia hapo nasema Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi maana kama kasisi upande huu mwengine ama mzee wa Kanisa, nasema mwili huu ni mavumbi na utarudi mavumbini. Ndugu zetu Waislamu pia wakasema *"kullu nafsi dhaika-tul maut"* (Kila nafsi itaonja mauti). Kwa hivyo haina budi tukubali lakini na uchungu. Mungu atubariki.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you.

Hon. Kilabo: Asante sana Bw Spika kwa kunipa hii nafasi nami kutoa rambirambi zangu. Natoa rambirambi zangu kwa mheshimiwa wetu ambaye ametuacha, mheshimiwa Chihanga. Kweli yaumiza lakini kweli haya ni mambo ambayo hatuwezi kuepukana nayo. Mheshimiwa Chihanga amekuwa ni mchangamfu sana na tumeona juhudi na bidii zake katika hili Bunge letu.

Namkumbuka mheshimiwa Chihanga majuzi tu tulipokuwa kule Eldoret yeye akiwa anacheza *netball* na mimi nikiwa ndiye mfunga lango wa kuvuta kamba na tulipovutwa na wale watu wote kuanguka nikabaki mimi, hakika nilianguka na nilipoanguka nilikuwa na maumivu siwezi kuondoka. Yeye alikuwa wa kwanza kuja kuniondoa; alikuwa ni mwema na mpenda amani.

Bw Spika, haya yote ambayo tunazungumza katika Bunge hili ni mambo ambayo yamekuja kwa sisi sote ambao tuko hapa. Tuweze kutoa heshima zetu na kutambua hususan nyumba hii mheshimiwa Chihanga akiwa ni mmoja wetu na ametuacha najua kuna changamoto nyingi lakini mimi mjumbe wa Sokoni Bw. Kilabo, ninasema mheshimiwa Chihanga kulingana na wakati huu ambapo ameaga, naomba Bunge lisitoe chochote katika mshahara wake mwezi huu apewe kamili. Nikizungumza hayo, najua tunakatwa pesa nyingi ambazo baada ya mfumo huu wa miaka mitano tungeweza kupata marupurupu yetu. Bw Spika, kama kuna kukatwa kwa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

hela zozote nisingetaka alivyotuacha kuwe na kukatwa kwa pesa hizo bali kama kuna pesa zozote zake ziandaliwe na kuna pia mtoto mmoja wa kiume ambaye yuko shule aweze kupewa.

Kilio ambacho kilinistaajabisha tukiwa sisi ni waheshimiwa na aliyekufa hapa ni mheshimiwa, pale nyumbani nilipokwenda kulikuwa na vilio vya watoto wakinirukia hata sijui walikuwa wananiita na jina la ‘*damage*’ nikasema haya mambo haya yametoka wapi?

(*Laughter*)

Lakini hii pengine ni changamoto yangu na ukakamavu wangu katika mikutano yangu ninaposimama na kuongea na watu kujua Kilabo anafanya kazi. Bw Spika, ikiwa itawezekana na naomba iwezekane, wale watoto mmoja wao yule ambaye yuko pale, msichana ambaye ana karatasi zake kama angeweza kupewa nafasi katika sehemu hii ya Bunge ama *Executive* kufanya ili kufuta majonzi. Ni heshima kuu na ni heshima kwa nyumba yetu.

Bw Spika, nasema pole na pole kwa mpendwa wetu mpenda amani. Tumetembea hapa na hapa na Kamati yetu ya Ardhi. Tulitembea kwingi kuomba Mungu kwenye ndege hapa na pale tukiwa pamoja na yeye. Tukishikana mikono tukiwa tunaingia ndani ya ndege na tukiona pengine lolote linaweza kutokea kwa uoga lakini hayo yote Mungu alituzuku. Tumefanikiwa tukaja naye pamoja mpaka hivi aje apatwe na kifo chake. Nasema pole na tutasimama imara na mazishi ya kufana na tuwe pamoja kwa harusi yake ya mwisho. Asante, Bw. Spika.

Hon. (Ms.) Elina: Asante Bw. Spika. Nami pia nimesimama kutoa rambi rambi zangu kwa mheshimiwa Chihanga. Kusema ule ukweli Bw. Spika, mheshimiwa Chihanga alivyoishi hapa kuna wengine watakuwa wagonjwa kwa sababu walikuwa karibu sana na Chihanga. Pengine leo watapata nafasi waseme ama hawatasema lakini najua wengine wako na maumivu moyoni. Chihanga alinipigia simu akiwa amelazwa pale hospitali ya Maimoon akaniambia “nimefanyiwa upasuaji jana mama, na ninaendelea vizuri lakini ningomba uje” kwa sababu, Chihanga nyumba ile ambayo anaishi kwa sasa ni yangu.

Nilipofika pale saa mbili usiku, nilimuona Chihanga ni kama amepona maana alikuwa mzima kabisa. Akaniambia “nilifanyiwa upasuaji jana na hivi naendelea vizuri, kilichobaki mimi nakohoa tu na kutapika lakini wamesema ni ile dawa waliyoniweka huenda ikanitapisha lakini nashukuru mama. Mungu akubariki sana.” Hii ni kwa sababu kuna kijana ambaye anatoka kwa Wadi yangu na ni shemegi yake akawa amemuita. Alikuwa hana namba yake, lakini akaniuliza nimpe namba ya huyo kijana. Nilipompatia ile namba ya yule kijana kumbe yule kijana ndio atakuja amsaidie Chihanga kwa kutoa damu; akatolewa damu akawekwa Chihanga. Akaniambia huyo kijana kama si ile namba uliyonipatia Voi, sijui ningefanyika nini lakini amenisaidia na damu. Nataka uregeshe salamu hizi mimi nikiwa niko hapa kitandani, mjulishe zaidi na wewe ujue ya kwamba namshukuru na Mungu amsaidie kwa kunisaidia kunipa ile damu yake.

Chihanga alikuwa ni mzima kabisa; kilichotekea baadaye ni kwamba Chihanga alibadilika tu kwa muda mfupi sana siku ya pili yake. Alipobadilika, ni kwamba ugonjwa ni kama umepanda kwa kichwa. Kila aliyeenda kumuona pale hakudhani kwamba Chihanga anaweza kutuacha.

Kila mtu hapa Bungeni tulikuja sisi sote kutoka Wadi tofauti tofauti lakini dada yetu Chihanga alipokuja hapa yeye kwanza alionekana ni kama ambaye anatoka sehemu za Malindi. Kila mtu alikuwa anampenda; hana mtu ambaye alikuwa ana chuki naye. Wacha sisi waheshimiwa, hata wafanyaji kazi wakati tulipoenda Eldoret tulikuwa tunacheza pamoja na

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wafanyi kazi, yeye alikuwa amejumuika na kila mtu. Roho ambayo alikuwa nayo Chihanga, sijui tuifanani na nani kwa sababu yeye vile alivyokuja hapa alikuwa ana umri mdogo lakini Chihanga alikuwa hawezi kukaa mahali kusengenya mtu kabisa.

Marehemu alikuwa ni mwana kamati wangu wa Michezo na hata mimi mwenywe nilikuwa nikichelewa kupata habari lakini yeye ataipata kutoka kwa kaunti nyingine ni kwamba safari iko tunaenda mahali fulani; alikuwa na bidii ile ambayo siwezi kuitajia mtu mwingine. Kusema ule ukweli, tumepoteza mama mheshimiwa Grace; si jambo zuri na jifikirieni wapendwa, leo twatoa rambi rambi za mwenzetu, sijui wewe utatolewa wapi lakini kusema ule ukweli, ule ugonjwa vile ulivyotutatanisha, mimi bado nikikaa namuangalia vile nilivyomuona akiwa hospitalini. Chihanga amekufa akiwa mzima yaani ameenda tu kirahisi sana maana wengine huumwa wakawa wagonjwa...

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you hon...

Hon. (Ms.) Elina: Mheshimiwa Spika, nimesimama kusema, tuwe pole sote na Mungu aliye mbinguni amuweke alipochagua mheshimiwa Chihanga. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you very much. Hon. Members the 20 minutes allotted have been all consumed and I know it's a very sad moment, given the opportunity I think we would eulogize her for the rest of the day but because we have a schedule to beat this afternoon, I kindly pray that we leave it at that and I am sure we will have another opportunity to talk about her. We will now go back to the normal Business of the House and for the Members who had made their requests to speak, kindly withdraw them so that we move to the normal business because my screen is full. Yes, we will move to the next Order.

PAPERS LAID

REPORT ON THE OPERATIONS AND FINANCIAL STATEMENTS OF KILIFI COUNTY FOR THE FINANCIAL YEAR 2013/2014

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes hon. Duncan Kaingu proceed.

Hon. Kaingu: Thank you so much Mr. Speaker, Sir. On behalf of the Members of the County Public Investments and Accounts Committee, I beg to table the Report on the financial operations of the Kilifi County Executive for the financial year 2013/2014, and the financial statements of the County Government of Kilifi for the year that ended 30th of June, 2014. Thank you.

(Hon Kaingu laid the Report on the Table)

REPORT ON COUNTY COMPLIANCE WITH VALUES AND PRINCIPLES

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Leader of Majority.

The Leader of Majority (Hon. Mwingo): Thank you Mr. Speaker Sir. I beg to lay the Report of the County Government of Kilifi Public Service Board on county compliance with values and principles in Articles 10 and 232 of the Constitution. Thank you, Mr. Speaker.

(Hon. Mwingo laid the Report on the Table)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

REPORT ON THE KILIFI COUNTY BUDGET ESTIMATES FOR THE 2016/2017
FINANCIAL YEAR

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Chair, you seem like you have seen a ghost. Are you ready?

Hon. Mangi: Mr. Speaker, I would wish to defer the tabling of this Report as I am making some final touches so that it is acceptable to all hon. Members. Thank you Mr. Speaker, Sir.

The Speaker (Hon Kahindi): When do you wish to have the same tabled? Remember we are working on a very tight schedule.

Hon. Mangi: I intend to table the Report before or on Wednesday Mr. Speaker, Sir.

The Speaker (Hon. Kahindi): Okay, I will allow you.

Hon. Mangi: Thank you Mr. Speaker, Sir.

(Tabling of the Report deferred)

STATEMENTS

STATUS OF KILIFI COUNTY RESOURCE MAPPING

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Foleni.

Hon. Foleni: Asante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza nataka kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuangalia Ripoti hii. Wiki iliyopita, nilipitia Ripoti hii kwa busara na nikaweka akili zangu zote katika ile Ripoti. Unafahamu Ripoti hii ni kubwa mno. Lakini nilienda nikaweka akili yangu yote katika ile Ripoti; nilikaa mahali na kuhakikisha kwamba nimeisoma ili hivi leo niambie Bunge hili kwamba Ripoti hii nimeikubali. Ninachooomba hata kama ni kubwa lakini ile kamati husika ipewe ili kuchambua kilicho ndani ili kuhakikisha Ripoti hii tunaweza kuigawanya na Serikali ya Kitaifa.

Hata ikiwezakana mheshimiwa waziri Dan Kazungu ambaye alichaguliwa juzi aweze kupata nakala hii. Nimegundua kwamba iwapo tutatumia Ripoti hii vizuri, basi tutapoteza njaa na umaskini na pia kupata nafasi za kazi kwa sababu katika Kilifi kuna madini mengi kulingana na hii Ripoti.

REQUESTS FOR STATEMENTS

MANAGING EROSION IN NGOMENI VILLAGE, GONGONI WARD

Hon. Kiraga: Mr. Speaker, this Statement is directed to the County Executive Committee Member (CEC) in charge of Environment and Natural Resources through the Chairperson Environment and Natural Resources Committee. The Statements reads as follows:

Is the CEC Member aware that Ngomeni village in Gongoni Ward has been experiencing sea, water and soil erosion and affecting the day to day activities of the village? What measure is the Department putting to stop erosion to the village?

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

STREET LIGHTING IN NGOMENI VILLAGE IN GONGONI WARD

I also have another Statement directed to the CEC Member in charge of Energy through the Chairperson, Energy Committee;

Is the CEC Member in charge of Energy aware that Ngomeni village in Gongoni Ward has no street/high mast lighting exposing it to security threats? Whether, he is aware that the village is located at the sea shore, and if yes, when shall a high mast light be installed in the village?

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you hon. Kiraga for your request for Statements.

BILLS

Second Reading

THE KILIFI COUNTY AGRICULTURAL DEVELOPMENT FUND BILL, 2016

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes hon. Gambo.

Hon. Gambo: Thank you. I beg to move that the Kilifi County Agricultural Development Fund Bill, 2016 be now read a Second Time. I call upon hon. Lali to second.

(Hon. Lali stood at his place to second)

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you. Hon. Members, a Motion has been moved by hon. Gambo to have the Kilifi County Agricultural Development Fund Bill, 2016 read for the Second time. I now propose that the same is ready for debate.

(Question proposed)

Yes hon. Lali.

Hon. Lali: Asante kwa nafasi hii. Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa katika gatuzi letu la Kilifi, asilimia 90 ya wakaazi wanategemea kilimo kama njia ya kupata lishe na kukimu mahitaji ya familia zao. Imekuwa ni changamoto kubwa kwa wakulima kuweza kulima na kupata mazao kwa sababu ya upungufu wa hela katika kupata pembejeo za kufanya kilimo kiwe cha kunufaisha. Wamejaribu katika kila njia waweze kupata pesa ili weweze kujikimu katika kilimo. Kumekuwa na mashirika yamewekwa pale na serikali ya Kitaifa, lakini sheria zilizowekwa wakulima wetu wengi hawawezi kusaidika kupitia sheria ili kupata pesa kununua pembejeo.

Serikali yetu ya kaunti imekuja na Sheria hii iliyo mbele yetu. Wananchi tumewapitishia Mswaada huu na wengi wamechangia wakipongeza sana gatuzi letu kwa kuja na sheria kama hii ili kuwapa wananchi mfuko wa kukopa pesa za kuwekeza katika kilimo ili kipanuke; wao wapate riziki, na serikali yetu ya Kilifi inufaike kutokana na mazao yatakayopatikana pale. Langu ni kuwaomba kwamba tupitishie Mswaada huu ili wananchi wetu wasaidike. Wananchi wameteseka kwa siku nyingi na imefika wakati, gatuzi letu limekuja na mfumo mwafaka ili wananchi wasaidike. Ni jukumu sisi waheshimiwa tupitishie ili sheria hii ifanye kazi kwa vile ambavyo tayari bajeti iko mbele yetu inapitishwa. Kwa hayo machache nasema asante sana.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you. Hon. Members, the Kilifi County Agricultural Development Fund Bill, 2016 has been moved to be read for the Second Time.

(Question put and agreed to)

Chairperson, please proceed.

Hon. Gambo: Thank you. I would like to give thanks to the Member who has supported the Second Reading of this Bill.

(The Bill was read a Second Time and committed to a Committee of the whole House at a later date)

THE KILIFI COUNTY ANTI-PORNOGRAPHY BILL, 2016

Hon. (Ms.) Elina: Mr. Speaker, I beg to move that the County Anti-Pornography Bill, 2016, be now read a Second Time. I call up on hon. Matano to second.

(Hon. Matano stood at his place to second)

The Speaker (Hon. Kahindi): Thank you. Hon. Member, the Motion to read the Kilifi County Anti-Pornography Bill, 2016, for a Second Time has been moved by hon. (Ms.) Elina Mbaru.

(Question proposed)

Yes, hon. Matano.

Hon. Matano: Asante sana, mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono kusomwa kwa sheria hii ya kudhibiti maswala ya ngono ndani ya kaunti yetu. Mheshimiwa Spika, tunapoangalia katika sheria hii tunayoitengeneza, itaweza kudumisha mila na destruti zetu maana maswala ya ngono yaliyoingilia katika kaunti yetu yameharibu na yameenda kinyume na desturi na mila zetu.

Tunavyoangalia ni kwamba maswala haya yanaendelea kutatiza hata vijana wetu katika elimu zao na maisha yao ambapo wameathirika kiakili na mambo yao na maswala yao mengi yameelekezwa katika maswala haya na filamu hizi. Basi kwa ajili ya haya nami nasimama kuunga mkono kusomwa kwa mara ya pili kwa Mswaada huu. Asante.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Members, a Motion to read The Kilifi County Anti-Pornography Bill, 2016, has been moved in order to have the Bill read a Second Time and the same has been deliberated.

(Question put and agreed to)

(The Bill was read a Second Time and committed to a Committee of the whole House at a later date)

ADJOURNMENT

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.

The Speaker (Hon. Kahindi): Hon. Members, in the absence of any other Business in the Order Paper, I move to adjourn this House until tomorrow 9.30 a.m.

The House rose at 3:55 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*